

Kufuata kundi la nyuki wa asali wa Kijapani

Sekta ya ufugaji nyuki ya Japani ina aina mbili za nyuki, nyuki wa Magharibi walioagizwa kutoka nje, na nyuki wa asili wa Kijapani. Nyuki wa Magharibi waliletwa Japani mwishoni mwa miaka ya 1800 na kushinda sekta ya ufugaji nyuki kutokana uzalishaji wao wa asali nyingi.

Walakini, ufugaji nyuki wa kienyeji nchini Japani unatekelezwa hadi leo. Mojawapo ya tofauti kuu katika ufugaji wa nyuki wa Kijapani ni jinsi tunavyopata kundi jipya. Pia uzalisha nyuki malkia ni changamoto kubwa sana, na pia huwezi kununua kundi la nyuki. Kwa hivyo, wafugaji hukamata makundi katika majira ya masika. Leo tutafuutilia kundi hili la nyuki waliotoroka kwenye mzinga wao karibu saa sita mchana siku iliyotangulia. Mzinga mpya ulitayarishwa kwa matumaini kwamba kundi hilo lingetulia pale, kwa hivyo tukaamua kuafuutilia. Makundi ya nyuki wa asali ya Kijapani mara nyingi hukaa kwenye mashimo matupu.

Kukamata kundi

Kundi hilo linakusanyika kwenye shimo. Inaonekana kundi hili linajaribu kutulia kwenye jengo hili la zege. Kizuizi cha zege kinaegemea nguzo ya chuma na kuna nyuki wachache ndani. Hii haionekani kama mahali pazuri pa kundi hilo kukaa. Ni muhimu kuliziba shimo hili ili kulinda nyuki dhidi ya wadudu. Changamoto lingine ni kwamba bomba la maji lilipo karibu na kundi litatatizwa na mtiririko wa maji. Pia jengo hilo la zege si kubwa vya kutosha, kwani nyuki watashambuliwa na upemo na mvua. Pia liko karibu sana na ardhi, hivyo itakuwa vigumu kwa kundi hilo kukua. Kwa hivyo tumia mzinga ili kutolea nyuki hawa makazi salama.

Kuhamisha kundi

Mzinga unaweza kutoa makao salama kwa kundi hilo. Nyuki hukamatwa kwa wingi iwezekanavyo na kuwekwa ndani mzinga. Tumia brashi mpya ili kuhamishia nyuki kwenye mzinga kwa urahisi. Kundi hutulia iwapo malkia yuko ndani ya mzinga, na

pia nyuki wengine kisha hufuata na kutulia kwenye mzinga mpya.